**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 10/11/2021**

**WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi.vije M.Ndwanga | Mwenyekiti. |
| 2. | Furaha L.Sarakikya | Katibu |
| 3. | Bw.Hoyange M.Mbwambo | Mjumbe. |
| 4. | Eng. Ramadhni S.Mtinge | Mjumbe. |
| 5. | Aisha Mhando | Mshauri |
| 6. | DR Flora Kessy | Mjumbe |
| 7. | Mr. Edward Mgaya | Mjumbe |

**SECRETARIETI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Pendo Vicent | PMU |
| 2. | Mandela Mhode | Field |
| 3. | Juma Saidi Mwalimu | Field |

**AGENDA:**

1. Kufungua Kikao
2. Kuidhinisha kutumia njia ya force akaunti kwenye ujenzi wa fedha za uviko -19
3. Kuongeza kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022 fedha za uviko
4. . Kujadili ujenzi wa madarasa 67 yaliyopata fedha za uviko -19
5. Kujadili ujenzi wa shule ya sekondari mpya ya Kilulu
6. Kuidhinisha manunuzi mbalimbali.
7. Kufunga Kikao

**MUHTA NA 1/11/2021 KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 12.20 mchana na kuwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria .

**MUHTA NA 2/11/2021 KUONGEZA KWENYE MPANGO WA MANUNUZI WA MWAKA 2021/2022 FEDHA ZA UVIKO.**

Katibu alitoa taarifa kuwa Halmashauri imepokea fedha kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya afya na elimu ambapo fedha hizo zimekusudiwa kujenga madarasa takribani 57 kwa shule za sekondari, madarasa 10 kwa shule za msingi, bweni 1 la wenye mahitaji maalumu pamoja na nyumba ya mtumishi wa afya. Hivyo basi katibu anaomba ridhaa ya kuongeza kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2021/2022 baada ya kupokea fadha ambazo zilikuwa nje ya bajeti .Wajumbe walijadili swala hilo na kukubaliana kuwa kiasi cha Tsh. 2,050,000,000

**MUHTA NA 2/11/2021 KUIDHINISHA KUTUMIA NJIA YA FORCE AKAUNTI KWENYE UJENZI WA FEDHA ZA UVIKO -19**

Katibu alitoa taarifa kuwa Halmashauri imetengewa Tsh. 1,510,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya afya na elimu. Hivyo kitengo cha manunuzi kinaomba kutumia njia ya force akaunti kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya afya na elimu kama ifuatavyo;

| SN | JINA KITUO KILICHOPATA MRADI | AINA YA MRADI | IDADI | KIASI KILICHO POKELE WA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | BEBERE PRIMARY | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 4 | 80,000.00 |
| 2. | BONDE SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi | 4 | 80,000.00 |
| 3. | BWEMBWERA SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 4. | CHIEF MANGENYA SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 3 | 60,000.00 |
| 5. | JAMBE PRIMARY | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 6. | KERENGE SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 7. | KICHEBA SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 8. | KIGOMBE SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 9. | KILULU SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 3 | 60,000.00 |
| 10. | KWABADA SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 11. | KWABUTU SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 12. | KWAFUNGO SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 4 | 80,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13. | KWEMKABALA PRIMARY | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 4 | 80,000.00 |
| 14. | KWEMKABALA SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 4 | 80,000.00 |
| 15. | MAGILA SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 16. | MISALAI SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 3 | 60,000.00 |
| 17. | MISOZWE SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 18. | MKURUMUZI SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 19. | MKUZI SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 20. | MLINGA SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 21. | MLINGANO SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 22. | MPAPAYU SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 23. | MTINDIRO SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 24. | NGOMENI SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 25. | NGOMENI MSINGI | ujenzi wa bweni kwa wenye mahitaji maalum | 1 | 80,000.00 |
| 26. | NKUMBA SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 27. | POTWE SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 28. | SHEBOMEZA SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 29. | SONGA SEC | ujenzi wa vyumba vya | 4 | 80,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | madarasa | | |
| 30. | TONGWE SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 31. | ZIGI SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 1 | 20,000.00 |
| 32. | ZIRAI SEC | ujenzi wa vyumba vya madarasa | 2 | 40,000.00 |
| 33. | HOSPITALI YA WILAYA | nyumba ya mtumishi | 1 | 90,000.00 |

Wajumbe walijadili taarifa hiyo na kukubaliana kuwa kazi hiyo itekelezwe kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na serikali.

**MUHTA NA 3/11 /2021 KUJADILI UJENZI WA MADARASA 67 YALIYOPATA FEDHA ZA UVIKO -19.**

Katibu alitoa taarifa alitoa taarifa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ni miongoni mwa Halmashari zilizopata fedha za kovid -19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa.

Aidha katibu alisisitiza kuwa Mkoa uliitisha kikao kilichowashirikisha Wakurugenzi,mhandisi wa ujenzi,mganga mkuu na maafisa elimu zote ambapo mkoa walisisitiza vifaa vinunuliwe kwa pamoja .

Awali Mkoa uliagiza Halmashauri kuwasilisha mahitaji ambayo yangenunuliwa kwa ujumla ambapo yaliwasilishwa lakini baada ya kikao cha Mkoa kilitoitishwa waliagiza baadhi ya vifaa kununuliwa kwa ujumla ikiwepo

- Saruji
- Mabati na kofia
- Matofali
- Nondo
- Mbao

Wajumbe walianza kujadili swala hilo kama ifuatavyo;

**Ununuzi wa saruji**

| S/N | JINA LA MZABUNI | GHARAMA |
|---|---|---|
| 1 | RAI SHOP ENTERPRISES | 130,365,500 |
| 2 | TANGA CEMENT | 131,689,275 |
| 3 | JAMES STEPHEN HIZA | 143,542,000 |

Katibu aliwasilisha taarifa kuwa baada ya kupokea maombi ya ununuzi wa saruji amefanya nukuu za bei kiwanda cha Tanga Cement na kwanda cha Maweni lime stone ambapo kiwanda cha maweni limestone kilimuelekeza kwenda kufanya nukuu za bei Rai Shop Enterprise ambaye ni Wakala wa kiwanda hicho kama mchanganuo unavyoonekana hapo juu. Wajumbe walijadili taarifa hiyo na kukubaliana kuwa kazi hiyo apewe Rai shop kwa kuwa kwa bei yake ni sawa na kuuza mfuko kwa gharama ya Tsh. 12,700 ambapo ni gharama ya kununua na kusafirisha pamoja na kushusha isipokuwa kwa kata ya Amani,Magoroto ,Misalai pamoja na Zirai ambapo saruji zao zingesafirishwa hadi Kata ya Kisiwani. Ambapo kama tukinunua tanga Cement ni sawa na Tsh.12,828.96 na wanasafirisha hadi makao makuu ya Halmashauri na gharama za kushusha ni Halmashauri.

- **UNUNUZI WA MABATI NA KOFIA**

  Katibu alitoa taarifa kuwa swala la ununuzi wa bati ameshaanza kufanya nukuu za bei na baada ya kukamilika kwa michakato ataiwasilisha kwenye kikao kwa ajili ya kuidhinisha manunuzi hayo.

- **UNUNUZI WA MATOFALI**

  Katibu aliwasisha taarifa miongoni mwa vifaa vilivyopitishwa kununuliwa kwa pamoja kwenye kikao cha Mkoa ni pamoja na tofali lakini bodi ya zabuni waliazimia kwa pamoja kuwa kulingana na jiografia ya Muheza kununua kwa pamoja italeta usumbufu hivyo walikubaliana kila mkuu wa shule asimamie ununuzi wa tofali kwa kuzingatia bei elekezi ya Tsh. 1400 kwa tofali isipokuwa wa shule za mbali zitatolewa ufafanuzi kwa kadri utekelezaji unavyoendelea isipokuwa kwa zile kata za amani.

- **UNUNUZI WA NONDO**

  Katibu alitoa taarifa kuwa swala la ununuzi wa nondo ameshaanza kufanya nukuu za bei na baada ya kukamilika kwa michakato ataiwasilisha kwenye kikao kwa ajili ya kuidhinisha manunuzi hayo.

- **UNUNUZI WA MBAO**

  Katibu alitoa taarifa kuwa kuna swala la ununuzi wa mbao kwa ajili ya ujenzi wa madarasa pamoja na bweni ,Wajumbe walijadili taarifa hiyo na kukubaliana kuwa swala la mbao kila shule wanunue isipokuwa ufuatiliaji wa ubora pamoja na bei ufuattiliwe kwa ukaribu ngazi ya Halmashauri.

Note ;Wajumbe kwa pamoja walikubaliana kwa pamoja kuwa vifaa vyote vya ujenzi wa madarasa vinavyonunuliwa ngazi ya Halmashauri vitengenezewe mkataba ambao utasainiwa na Mkurugenzi

mtendaji na Mwenyekiti wa Halmashauri ambapo kila shule itapewa invoice na delivery kwa ajili ya kufanya malipo ikiambatana na huo mkataba.

MUHTA NA 4/11/2021 . KUJADILI UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI MPYA YA KILULU

Katibu alitoa taarifa ya ujenzi wa shule mpya ya Kilulu ambapo alisema hatua ya msingi imekamilika na kwa sasa hatua inayofuata ni umwagaji wa zege la jamvi lakini changamoto kubwa inayoukabili mradi huo ni upatikanaji wa maji.

Wajumbee waliitaji mhandisi alitolee ufafanuzi jambo hilo ambapo alisema awali walifikiri kupamp maji yaliyokuwa bondeni lakini ilishindikana kutokana na maji hayo kuwa madogo na pia alitoa ufafanuzi kuwa amejaribu kuwasiliana na tanga uwasa pamoja na wadau wengine wanachimba visima virefu na kupata gharama ya uchimbaji inazidi milioni ishirini na tano ,

Hivyo alishauri tuchimbe visima viwili vya mkono ambapo vitasaidia utekelezaji wa mradi huo. Wajumbe walijadiliana taarifa hiyo na kukubaliana kuwa watafutwe watu kwa ajili ya kuchimba visima hivyo kwa uharaka.

**MUHTA NA 5/11/2021 KUIDHINISHA MANUNUZI MBALIMBALI**

- **Ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa hospitali ya Wilaya**
  -Ununuzi wa saruji Rai Shop Enterprise Tsh. 3,810,000/=
  -Ununuzi wa vifaa vya ujenzi James Stephen Hiza Tsh. 6,822,000/=
  - Ununuzi wa mbao James Stephen Hiza Tsh. 7,920,000
- **Vifaa vya nyongeza kwa ajili ya eneo la kufyatulia Tofali**
  - James Stephen Hiza Tsh 3,189,400/=
  -Aniset Kalist Marandu Tsh. 2,450,000/= vifaa vya umeme
  -Vifaa vya mabomba James Stephen Hiza Tsh. 145,000/= vifaa vya mabomba
- **Ununuzi wa pikipiki pamoja nashajala**
  -Ununuzi wa shajala Nyampande Investment Tsh. 2,060,000/=
  -Ununuzi wa pikipiki Motries Investment Tsh. 16,980,200-Aitwe kwa ajili ya majadiliano

**MUHTA NA 6/11/2021 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 2.40 jioni na kuwashukuru wajumbe kwa michango yao na kuwatakia utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA

**VIJE NDWANGA**
SAHIHI-----------------------

MWENYEKITI

**FURAHA L. SARAKIKYA**
SAHIHI-----------------------

KATIBU

TAREHE 10/11/2021